JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

SHULE YA SEKONDARI BIHAWANA

S.L.P 934, DODOMA ***EMAIL: bihawana.sec@dodomacc.go.tz***

Simu:0744 000 220, 0784 934 602 , 0768 271 266

Mawasiliano shuleni piga:

0744 000 220

0782 770 290

0784 934 602

0768 271 266

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI .....
S. L. P .....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI BIHAWANA 2021/2022

1.0 **UTANGULIZI:**

Nachukua fursa hii kukupongeza na kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga Kidato cha tano katika shule hii kwa mwaka 2021/2022 mchepuo wa ……

Soma kwa makini taarifa na maelekezo ya kujiunga na Shule, kisha jaza fomu maalum zilizoambatanishwa na kulipia ada na michango mingine kabla ya kuripoti shuleni.

Hakikisha unakuja shuleni na fomu tulizokutumia zikiwa zimejazwa kikamilifu.

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti **tarehe .....**

1.1 Mahali Shule ilipo.

Shule ipo umbali wa kilometa 18 kutoka Dodoma mjini ikitanguliwa na Bihawana Seminari na Kituo cha Kilimo cha Bihawana. Kutoka stand ya Basi ya mkoa– DODOMA, panda Daladala ziendazo **Sabasaba (mjini)**Tshs 400/, kisha panda daladala ziendazo **Kikuyu stand mpya(stand ya gari za Mkonze)** (Tsh 500) Hapo ndipo utapata magari ya kwenda Bihawana (nauli Tsh 1000). Au (chukua bajaji au bodaboda kutoka stand ya mabasi hadi Stand Mpya Kikuyu).

2.0 Lengo la shule:

Shule ya sekondari Bihawana ina malengo ya jumla yafuatayo:

(i) Kuwahimiza vijana kupenda kusoma kwa bidii na kutii sheria za Shule bila kushurutishwa.

(ii) Kuwaelimisha na kuwalea vijana wa Kitanzania kuanzia kidato cha Tano hadi cha Sita kuwa wakakamavu, wazalendo na raia wema wasiohitaji kusukumwa katika kutenda kazi mbalimbali.

(iii) Kuwaandaa vijana kuwa viongozi wa kutegemewa na jamii ya Kitanzania Taifa na dunia kwa ujumla.

3.0 Masomo yanayofundishwa katika shule hii ni:-

(i) General Studies
(ii) English Language
(iii) History
(iv) Geography
(v) Basic Applied Mathematics
(vi) Biology
(vii) Chemistry
(viii) Physics
(ix) Agricultural Science
(x) Advanced Mathematics

4.0 Ada ya Shule na michango mingine:

4.1 Ada ya Shule.

- Ada ya Shule kwa mwaka ni Tshs 70,000/= (Elfu Sabini tu) ambayo italipwa aidha kwa mkupuo mmoja au kwa mikupuo miwili kama ifuatavyo:
- Mkupuo wa kwanza Tshs 35,000/= kabla ya kuripoti Shuleni.
- Mkupuo wa pili Tshs 35,000/= kabla au tarehe 04/01/2022

4.2 Michango mingine unayotakiwa kulipa

Mwanafunzi anatakiwa kulipiwa michango mingine kabla ya kuripoti shuleni kama ifuatavyo:

- Ukarabati wa samani 15,000/= kwa kila mwaka
- Kitambulisho 6,000/=
- Uboreshaji wa taaluma 20,000/= kwa kila mwaka
- Wapishi, walinzi na vibarua wengine 20,000/= kwa kila mwaka
- Nembo ya shule 4000/=
- Fedha ya huduma ya kwanza na bima/CHF 15,000/= kwa kila mwaka
- Kukodisha godoro 20,000/= kwa mwaka
- Fedha ya Tahadhari 5000/=

MUHIMU: Malipo ya ada yalipwe kupitia Benki ya NATIONAL MICROFINANCE BANK (NMB) Tawi lolote nchini kwa jina la **BIHAWANA SECONDARY SCHOOL**A/C Na **5050 1100 168** na michango mingine yote ilipwe kupitia Benki hiyohiyo ya NATIONAL MICROFINANCE BANK (NMB) Tawi lolote nchini kwa jina la **BIHAWANA SEKONDARI- EK** A/C Na **5051 0010 302** na 'Pay in Slips' zote halisi (Original) za benki ziwasilishwe shuleni. Hakikisha jina la mwanafunzi linaandikwa kwenye hizo Pay in Slips.

Ada na michango mingine zikishalipwa **hazitarudishwa** kwa sababu yoyote ile. Malipo yote ni lazima yalipiwe benki, Shule haitawajibika kwa atakayelipa ***fedha taslim*** kwa mtu yeyote Yule.

5.0 Sare Rasmi za Shule.

5.1 Mashati mawili (02) meupe kitambaa cha Tetron **Mikono Mirefu** zenye mfuko mmoja .

5.2 (a) Suruali nne (04) Nyeusi zilizoshonwa vizuri zenye marinda mawili na mfuko mmoja wa nyuma usio na zipu na pindo la chini (turnup) la upana wa inchi 22 **(Suruali zilizobana (modo) hazitaruhusiwa)** na Mkanda Mweusi wa ngozi.

(b) Nguo za kushindia Fulana (T.Shirt) mbili (02) za mikono mifupi rangi ya **kijivu zenye kola** zisizo na maandishi.

5.3 Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba vya kufunika miguu (weusi uwe pia katika soli, kamba na ngozi).

5.4 Soksi nyeupe fupi jozi nne (04) zisizo na pambo lolote.

5.5 Sweta rangi ya kijani jeshi(dark green) mikono mirefu .

5.6 Track suit **ya light bluu** yenye michirizi myeupe mikononi na miguuni (***USIJE NA JEZI***)

5.7 Raba jozi moja.

ZINGATIA:Nguo ambazo sio sare ya shule haziruhusiwi shuleni. ukaguzi utafanyika wa vifaa/vitu vyote vitakavyoletwa shuleni. Ukipatikana na vifaa/nguo zisizohitajika utalazimika kuzirudisha nyumbani. Mwanafunzi aripoti shuleni akiwa amevalia sare.

6.0 VIFAA VYA SHULE.

6.1 Mahitaji muhimu ya Shule ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni

Mwanafunzi ni lazima alete mahitaji haya muhimu kwa uongozi wa Shule kabla ya kuruhusiwa kuanza/kuendelea na masomo hapa shuleni:

(i) Cheti cha Daktari wa Serikali (Ijazwe Fomu iliyoambatanishwa na maelekezo ya kujiunga na Shule).

(ii) Ijazwe kikamilifu fomu ya utambulisho na historia ya mwanafunzi (iliyoambatanishwa) ya wazazi 2 na walezi 2 watakaotambuliwa rasmi na shule.

(iii)Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa.

(iv)Ijazwe kikamilifu kiapo cha kutofanya migomo, fujo au kosa la jinai.

(v) Picha nne (04) za Passport Size(zenye shati jeupe).

(vi) Nakala ya Cheti cha kuhitimu kidato cha Nne (IV) au 'Result Slip'.

(vii) Photocopy Paper A4 (Rimu moja (01) kwa kila muhula.

(viii) Dawa ya chooni aina ya **ARO au CARELINE** .

(ix) Fedha za matibabu za kutosha.

(x)**Fagio la chelewa refu lenye mpini kwa Kila mwanafunzi**

- Squizer kwa wanafunzi wa CBG.

- Fagio laini la ndani (soft broom) na panga kwa wanafunzi wa HGL.
- Jembe na mpini wake kwa wanafunzi wa CBA na PCB.
- Fagio ngumu ya kusugulia chooni (Hard brush) kwa wanafunzi wa PCM.

6.2 **Vifaa Muhimu vya Darasani.**

(i) Begi la kutunzia / kubebea madaftari na vitabu (liwe la heshma).

(ii) Madaftari makubwa ya kutosha kulingana na masomo.

(iii) 'Ruler', Kalamu na mkebe wa vifaa vya hisabati (Mathematical set).

(iv) Vitabu vya kiada (text books) na Ziada (Reference Books) kulingana na mchepuo wa mwanafunzi.

(v) 'Scientific Calculator' moja (01) kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi.

(vi) Dissection kit 1 (kwa wanafunzi wanaosoma biology)

NB: Mzazi unashauriwa kumnunulia mwanao angalau kitabu kimoja kwa kila somo alilochaguliwa kusomea.

6.3 Vifaa vya Bweni

(i) Sahani ya chakula, bakuli, kikombe na kijiko.

(ii) Ndoo mbili za lita 10 za plastiki kwa kuogea na kufulia na kidumu cha lita 5 cha kuhifadhia maji ya kunywa.

(iii) Shuka tatu (03) zisizo na maandishi za rangi ya bluu na foronya yake na mto.

(iv) Taulo ya kuogea na mkebe wa kuwekea sabuni ' Soap Dish'.

(v) Chandarua kimoja cha mbu kilichowekwa dawa ya kuzuia malaria.

(vi) Nguo za ndani za kutosha (**Angalau tano**) sio bukta za michezo

(vii) Sabuni za kutosha za kuogea na kufulia.

(viii) Sanduku imara la **chuma moja tu** kwa ajili ya kutunzia nguo,vitabu n.k.

(ix) Viatu vya wazi (open shoes) sandles

6.4 Uandikishwaji na Usajili kwa mwanafunzi.

Siku ya kwanza ya kuripoti kila mwanafunzi awe na vitu vyote kama vilivyoagizwa

7.0 KAZI ZA NJE YA DARASA.

Kufanya kazi kwa bidii ndani na nje ya darasa ni katika nidhamu ya kijana wa Kitanzania anayotakiwa awe nayo, hivyo kila mwanafunzi atawajibika kushiriki kikamilifu katika kutenda kazi za usafi wa mazingira, miradi na kazi nyingine kama atakavyoelekezwa na viongozi wa wanafunzi na walimu. Kutega kazi iwe ya darasani au nje ya darasa ni kukiuka maadili yasiyotarajiwa kijana huyu awe nayo, na ni tabia ambayo haitovumiliwa kabisa.

8.0 SHERIA, KANUNI NA MWENENDO BORA WA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978** na inazingatia miongozo inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Aidha, wanafunzi wote wanatakiwa kuzingatia haya yafuatayo:

8.1 Unapojiunga na Shule.

Kila mwanafunzi anayejiunga na shule hii anapaswa kutambua kuwa yupo hapa kwa ajili ya **KUSOMA** kwa faida yake (familia yake) na Taifa lake kwa ujumla. Kwa sababu hiyo, chochote kilichopo nje ya jukumu hili hakina nafasi katika shule hii, kiwe kwa maneno au kwa vitendo.

8.2 Kuwahi na mahudhurio ya kila siku.

(i) Kuwahi shuleni ni wajibu wa kila mwanafunzi, hivyo kila mwanafunzi anapaswa kuripoti shuleni tarehe ya kufungua shule bila kukosa na kuendelea kuwepo shuleni kila siku.

(ii) Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na nje ya darasa. Vipindi vya kazi za mikono pamoja na michezo ni sehemu ya masomo. Ni wajibu pia kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine atakazopewa na Shule.

(iii) Wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria mikusanyiko halali yote ya shule kama vile, mstarini, usafi, Baraza la shule, Ibada, midahalo (Debates), n.k.

(iv) Ni lazima kutimiza kwa makini mahudhurio ya maandalio ya jioni (Evening Preparation).

(v) Ni lazima mwanafunzi ahifadhi vitu vyake na kulala bwenini. **'Bed Check'** na '**Inspection'**ukaguzi utafanyika mara kwa mara na wakati wowote bila taarifa.

(vi) Kila mwanafunzi anawajibika kuwahi kula chakula kwa wakati uliopangwa. Ni marufuku kuwahi kuchukua chakula kabla ya wengine wote, labda kwa kibali maalum. Tatizo lolote liripotiwe kwa mwalimu wa zamu / wa chakula kwanza.

8.3. Sare za Shule.

(i) Wanafunzi wote ni lazima kuvaa sare ya shule na kitamulisho cha shule muda wote wa darasani na anapotoka nje ya shule, tunasisitiza kuwa **suruali zilizobana (modo) na zisizo na marinda** hazitaruhusiwa kamwe.

(ii) Mwanafunzi lazima ajiweke katika hali ya usafi kimwili na kimavazi. Nguo zote atakazovaa mwanafunzi lazima zikubaliwe na uongozi wa shule, pale anaporipoti mwanafunzi shuleni awe amevaa sare za shule (rejea kifungu 5).

8.4. Heshima na Utii.

(i) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema popote alipo ndani na nje ya mipaka ya shule.

(ii) Kila mwanafunzi anatakiwa kutii keng Mwanafunzi anatakiwa kusimama /kumpokea na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita au aingiapo shuleni, darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

(iii) Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, fedha za Taifa, Wimbo wa Taifa, Wimbo wa Shule, Nembo ya Taifa na Picha za viongozi wa Serikali.

(iv) Wanafunzi wakati wote wawe na heshima kati yao wenyewe na kwa walimu na wafanyakazi wasio waalimu pia. Hairuhusiwi kwa wanafunzi kugombana au kufanya malumbano ya kidini, kikabila au mfano wa hayo.

(v) Kiranja yeyote wa shule anatakiwa kula kiapo cha utii na kuwa mfano katika kutekeleza kanuni na taratibu za shule. Kukiuka taratibu za shule kunaweza kumpotezea sifa ya kuwa kiongozi na adhabu nyingine kuchukuliwa dhidi yake ikiwa pamoja na kusimamishwa / kufukuzwa shule. Mkuu wa shule ana mamlaka ya kuteua kiongozi mwingine wakati wowote pale itakapobidi.

8.5. Sehemu muhimu za Kujifunzia kama madarasa, Maabara na Maktaba.

(i) Madarasa, Maabara na Maktaba ni sehemu za masomo, hivyo ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga kelele, kuzomea, kupiga gumzo au kuzurura ndani ya sehemu hizo. Hairuhusiwi kutumia viti na madawati kusomea nje ya madarasa au ukumbi wa mkutano bila ya kibali. Ikithibitika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa.

(ii) Ni marufuku kuingia kwenye Maabara bila ya kibali cha mwalimu husika.

(iii) Ni lazima kila mwanafunzi atumie Maktaba kufuatana na sheria za maktaba.

(iv) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuandika ubaoni bila ya kibali cha mwalimu. Ni vyema mbao zote zifutwe baada ya kila kipindi au muda wa darasa unapokwisha.

9. AFYA.

Kila mwanafunzi lazima ajiweke katika hali nzuri ya kiafya ili aweze kuyamudu masomo yake vema.

(i) Mwanafunzi mwenye Ugonjwa hatari wa kuambukiza ni lazima atibiwe na kupona kabla ya kufika shuleni na taarifa ya kimaandishi ifikishwe shuleni haraka.

(ii) Mwanafunzi mwenye ugonjwa kama vile; Pumu, kifua kikuu, ugonjwa wa moyo lazima athibitishwe na Daktari ambaye atamshauri mgonjwa na shule kwa maandishi.

(iii) Endapo mwanafunzi ataugua ataomba ruhusa kwa mwalimu wa zamu/ mwalimu mshauri wa wanafunzi kama ataruhusiwa kwenda hospitali atatakiwa kurudi siku hiyohiyo. **Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na Mkuu wa Shule tu.**

(iv) Kila mwanafunzi ni lazima apimwe afya yake kabla ya kujiunga na shule na wakati wowote shule itakapoona kuna haja na umuhimu wa kufanya hivyo.

(v) Kila mwanafunzi hatakiwi kuchafua mazingira ya shule kwa namna yoyote ile mfano kutupa taka ovyo, kukatisha kwenye viunga vya maua, kwenda haja kubwa na ndogo mahali pasipostahili n.k. kufanya hivyo kunaweza kupelekea adhabu kali zaidi.

(vi) Kila mwanafunzi anapaswa kutunza mwili wake ikiwa pamoja na kukata kucha, nywele usawa wa unene wa ‘njiti ya kibiriti’ na kunyoa ndevu, kutandika kitanda, kuoga, kupiga mswaki, na kupanga vitu vizuri bwenini n.k. Hairuhusiwi kufuga ndevu, kuvaa pete, cheni, hereni, na mipira yoyote (mfano wa hayo) mikononi.

(vii) Ni lazima kila mwanafunzi kula chakula cha shule ’Mesini’ na maeneo yaliyo karibu na Mesini yaliyoruhusiwa na shule. Nimarufuku mwanafunzi kula chakula nje ya maeneo hayo kama Mabwenini, n.k. na marufuku pia kula au kuingiza chakula toka nje ya mipaka ya shule.

(viii) Ni marufuku wanafunzi kulala wawili kwenye kitanda kimoja.

MUHIMU: Wanafunzi wenye Bima ya Afya wanahimizwa kuja na kadi zao na watazionyesha wakati wa kuripoti

10 Mipaka ya Shule.

(i) Mwanafunzi yeyote atakayetoka nje ya mipaka ya shule lazima apate kibali cha Mwalimu wa zamu.

(ii) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea sehemu zifuatazo:

(a) Vilabu vya pombe au kunywa pombe, kuvuta sigara na madawa ya kulevya kama bangi, kubeli, Cocaine n.k.

(b) Majumba ya starehe (Bar, kumbi za muziki n.k).

(c) Nyumba za kufikia wageni (Lodging/Guest House).

(d) Nyumba za walimu ila kwa kibali / taarifa maalum.

11. Vifaa na Mali ya Shule.

(i) Majengo ya shule, Samani, Vifaa vya kazi na vifaa vya masomo ni mali iliyogharimu fedha nyingi sana, hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kuvitunza vizuri ili viweze kudumu kwa manufaa ya leo na kesho.

(ii) Ni marufuku kuandika au kuweka alama /chata katika kuta, milango, madirisha, meza au dawati au kiti na vitu vingine ambavyo ni mali ya shule.

(iii) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutoa taarifa kwa kiongozi /mwalimu mara tu uharibifu/kuvunja kifaa chochote cha shule unapotokea.

(iv). Uharibifu wowote au upotevu wa kitu chochote cha shule lazima ufidiwe badala yake.

(v) Mali zote za shule utakazokabidhiwa utalazimika kuzirudisha zikiwa katika hali nzuri, vinginevyo utalipia uharibifu.

12. Adhabu.

Mwanafunzi atakayevunja taratibu na kanuni hizi na zile ndogo za shule atapata adhabu husika kulingana na uzito wa kosa ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:

(i) Kuonywa na serikali ya wanafunzi au waalimu na akirudia kufanya kosa atapewa adhabu kali ikiwamo kazi za mikono.

(ii) Mwanafunzi akionekana haonyeki kesi yake itapelekwakwenye kikao cha kamati ya nidhamu ya shule, bado habadiliki atapelekwa kwenye Bodi ya shule na mzazi/mlezi atajulishwa

13. Makosa ambayo yanaweza kumfukuzisha shule mwanafunzi.

a. Kumiliki au kukutwa na simu ya Mkononi. ikikamatwa kwanza haitarudishwa kabisa kwa sababu yoyote ile na pia hatua nyingine kuchukuliwa kama vile kufukuzwa shule.
b. Wizi.
c. Uasherati/ubakaji/ushoga au vyote kwa pamoja.
d. Ulevi wa aina yoyote au uvutaji wa sigara, bangi na madawa ya kulevya.
e. Kupiga au kupigana.
f. Kugoma (mfano kutokula chakula cha shule), kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
g. Kuharibu mali ya shule/umma.
h. Kumpa mimba au kushiriki kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
i. Kuoa/kuolewa.
j. Kudharau Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa, Fedha za Taifa, Wimbo wa Taifa au picha za Viongozi wa serikali.
k. Utoro wa shule, mahudhurio mabovu darasani au kukosa kufanya mitihani/majaribio/mazoezi bila taarifa au kibali maalumu cha Mkuu wa Shule.
l. Kufanya makosa mengine ya jinai au uhaini kama vile kumiliki Baruti, Silaha za moto na mfano wa hayo.
m. Kukataa adhabu ya mwalimu, kugomea au kumtukana mwalimu au mtu yeyote.
n. Kuchelewa kufika shule, au kukosa kuwepo shuleni kwa siku 90 mfululizo bila taarifa rasmi.
o. Kuwa na nguo ambazo sio sare rasmi ya shule.

TANBIHI: Mwanafunzi atapewa adhabu ya kusimamishwa shule na kikao cha kamati ya nidhamu chini ya uongozi wa Mkuu wa shule na taarifa zitawasilishwa kwenye bodi ya shule.

Hata hivyo sheria za shule zinaweza kubadilika kulingana na mazingira/jamii kwa ujumla.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI BIHAWANA

JOSEPH MBILINYI
MKUU WA SHULE.

UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI KUKUBALI NA KUTII

SHERIA ZA SHULE

Mimi mwanafunzi (Jina kamili) ……

Nimezisoma sheria, kanuni na mwenendo bora wa shule kwa makini na kuzielewa. Nakubali kuzitii na kuzitekeleza zote kama zilivyo.

Sahihi ya mwanafunzi:…….Tarehe: ……..……

UTHIBITISHO WA MZAZI /MLEZI WA MWANAFUNZI KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE

Mimi ……ambayeni Mzazi /Mlezi wa mwanafunzi huyu, nimezisoma na kuzielewa kanuni, taratibu na mwenendo bora wa shule na kuzikubali kama zilivyo na nipo tayari kushirikiana na Shule katika kuzitekeleza kanuni, taratibu na sheria hizo na ninaahidi kumpatia vifaa na mahitaji mengine muhimu kama yalivyotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule na nathibitisha kwamba ndugu na jamaa nimewajaza kwenye fomu ya utambulisho iliyoambatanishwa na fomu hii.

Sahihi ya mzazi/mlezi (mdhamini 1) :…….…….

Tarehe:……, Namba za Simu;……

Sahihi ya mzazi/mlezi (mdhamini 2) :…….…….

Tarehe: ……,Namba za Simu;……

N.B. Ndugu ambaye hakutambulishwa, hatatambuliwa na uongozi wa shule, pindi anapohitajika mzazi/mlezi kwa masuala ya kinidhamu.

UTHIBITISHO WA SERIKALI YA MTAA NA KATA ANAPOTOKA MWANAFUNZI

1. **MWENYEKITI WA MTAA/KIJIJI(Simu……)**

   Mimi ……(Jina) ambaye ni …… (Cheo),

   nathibitisha kuwa kijana ……(Jina la mwanafunzi) anatoka katika mtaa/Kijiji wangu/changu na ni RAIA/SI RAIA WA TANZANIA.

   Sahihi:……. Tarehe:…… Muhuri wa Ofisi……..….

2. **MTENDAJI KATA (Namba ya simu……**

   Mimi ……Jina) ambaye ni ……....(Cheo),

   Nathibitisha kuwa kijana …….....(Jina la mwanafunzi) anatoka katika KATAyangu na ni RAIA/SI RAIA WA TANZANIA.

   Sahihi:……....., Tarehe:……....., Muhuri wa Ofisi.....…….

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

SHULE YA SEKONDARI BIHAWANA

S.L.P 934, DODOMA ***EMAIL: bihawana.sec@dodomacc.go.tz***

Simu:0784 934 602, 0744 000 220, 0768 271 266

FOMU YA UTAMBULISHO WA WAZAZI / WALEZI WA MWANAFUNZI

JINA …….……KIDATO:……. MCHEPUO:……...

WAZAZI

(a) Jina kamili la Baba:……

Anuani :…….. Simu:……

E-mail:…….. uhusiano(Baba):……..

Sahihi:…… Tarehe:…….

Picha ya hivi karibuni

(b)Jina kamili la Mama:……

Anuani :…….. Simu:……

E-mail:…….. uhusiano(Mama):……..

Sahihi:…… Tarehe:…….

Picha ya hivi karibuni

WALEZI

(a) Jina kamili la mlezi:……

Anuani :…….. Simu:……

E-mail:…….. uhusiano:……..……

Sahihi:…….…… Tarehe:……

Picha ya hivi karibuni

(b) Jina kamili la mlezi:……

Anuani :…….. Simu:……

E-mail:…….. uhusiano:…….……

Sahihi:…… Tarehe:…….

Picha ya hivi karibuni

NB:*Wazazi na walezi ni muhimu mjaze fomu hii kwa usahihi na ukamilifu. Ninyi ndio mtakaotambuliwa rasmi na Shule.*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

SHULE YA SEKONDARI BIHAWANA

S.L.P 934, DODOMA ***EMAIL: bihawana.sec@dodomacc.go.tz***

Simu:0784 934 602, 0744 000 220, 0768 271 266

MKATABA NA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI KUTOSHIRIKI MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi ……..……KIDATO:……. MCHEPUO:……...

Ninathibitisha kuwa nimewahi/sikuwahi kushiriki mgomo shule ya …… mwaka ……. Ninaahidi kutokufanya mgomo, fujo au kosa lolote la jinai kwa muda wote nitaokuwa Bihawana sekondari

Endapo nitajihusisha na migomo, fujo au kosa lolote la jinai niko tayari kufukuzwa shule.

Ukiwa mwanafunzi mwema eleza utafanya nini endapo utapata tetesi za mgomo, fujo au makosa mengine ya jinai hapa shuleni…….

……
……..

Jina ……. Sahihi ……

UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI/NDUGU

Mimi …… ambae ni Mzazi/mlezi/ndugu wa ……..

Nathibitisha kuwa kwa ufahamu wangu huyu kijan aliwahi/hakuwahi kushiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi kutoa ushirikiano kwa shule muda wote nitakapohitajika.

Jina …… Sahihi ……..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

SHULE YA SEKONDARI BIHAWANA

S.L.P 934, DODOMA ***EMAIL: bihawana.sec@dodomacc.go.tz***

Simu:0784 934 602, 0744 000 220, 0768 271 266

HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi …… dini/Dhehebu…….....
2. Jina kamili la baba ……
3. Namba za simu za baba zinazopatikana muda wote……..
4. Je baba yupo hai au amefariki ……...
5. Kama amefariki taja tarehe au mwaka aliofariki……...
6. Jina kamili la mama……...
7. Namba za simu za mama zinazopatikana muda wote……
8. Je mama yako yupo hai au amefariki…….
9. Kama amefariki taja tarehe au mwaka aliofariki……...
10. Anuani ya mzazi ……...
    S.L.P ……..
11. Kazi aifanyayo baba ……..
12. Sehemu anayofanyia kazi……..
13. Kazi aifanyayo mama ……...
14. Sehemu anakofanyia kazi……..
15. Kama huishi na mzazi wako taja jina la mlezi wako ……
16. Kazi aifanyayo……...
17. Sehemu anakofanyia kazi……..
18. Anuani ya mlezi ……
    S.L.P …… namba ya simu ……...
19. Habari nyingine za familia:
20. Jina la Kaka/Dada Umri kazi yake mahali anapofanyia kazi. Kama ni . mwanafunzi taja shule.
    (a)…… …..… …… ……
    (b) …… …… …… ……
21. Afya ya mwanafunzi (tafadhali eleza kama una ugonjwa wowote ambao una kukabili kwa hiyo unastahili huduma muhimu) Ni muhimu umfahamishe Daktari atakayekupima ili naye aweze kujaza katika sehemu inayomhusu kwenye fomu kwa ushauri zaidi wa kitaalamu……
    ……
22. Uthibitisho wa mwanafunzi:
    Nathibitisha kuwa maelezo niliyoandika katika fomu hii ni sahihi.

    Sahihi…….

    Tarehe ……..

_____

JOSEPH MBILINYI

MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

SHULE YA SEKONDARI BIHAWANA

S.L.P 934, DODOMA ***EMAIL: bihawana.sec@dodomacc.go.tz***

Simu: 0784 934 602, 0744000220, 0768 271 266

Date:……

REGIONAL /DISTRICT MEDICAL OFFICER,

P.O.BOX……...

…….

RE: MEDICAL EXAMINATION FORM

Admission to BIHAWANA SECONDARY SCHOOL is conditional upon receipt of this filled medical examination form. Kindly, you are requested to examine the mentioned below pupil with his current health status.

NAME OF EXAMINEE :…….. AGE:……

1. PERSONAL HISTORY

Has the examinee suffered from any of the following? If YES indicate date and diagnosis. If NO please write 'NO' in appropriate place.

(a) Tuberculosis……

(b) Other respiratory diseases…….…….

(c) Gastro-intestinal disease……..

(d) Renal or Genital Urinary disease…….

(e) Emotional disease or Psychosis……

(f) Serious Injuries……

(g) Any operations……

(h) Any fits……..

(i) Leprosy……

2. PHYSICAL EXAMINATION

(a) Height……..…… Weight……

(b) Ears……

(c) Eyes: Conjunctive …….

Pupils;……..
Rights;…….…….

(d) Ears (if any discharge)……

(e) Skin diseases……

(f) Mouth and throats:……...

(g) Nose:……

(h) Respiratory System: Any abnormality?.....

(i) Cardiovascular system: Blood Pressure : Systolic:…….……..

Heart: Any Murmur:……..

Arteries and Veins:……..

(j) Upper and Lower extremities……

(k) Abdomen:……..

Sears (Operation)……

Hernia:……

Hydrocele:……

Masses:……

Rectum:…….……...

Any Clinical evidence of hyperacidity or gastric duodenal ulcers:…….

3. LABORATORY

(a) Urine : Albumin……

Sugar:…….

Leuococytes:……..

Bilharzia……

(b) Stool:……

(Special emphasis on Hookworm and Bilharzia)

(c) Blood examination (any problems like Malaria etc)…….……

4. REPORT

I have examined Mr. …….. and consider that he is /not fit to be admitted to Bihawana Secondary School.

Name:…….
Signature:……..

Title:……Qualification:……

Official Stamp: Date:……